NAMBA YA KITAMBULISHO CHA MWANAFUNZI ____________

# Tunahitaji usaidizi wako!

## ...na tutakulipa kwa wakati wako.

**Successful Families 2020** ni juhudi ya pamoja kati ya mashirika yasiyokuwa ya biashara ya IRCO, Latino Network, Metropolitan Family Service, NAYA Family Center na SEI yanayo jitihadi kuimarisha matokeo ya elimu kwa wanafunzi wasiokuwa weupe kwa kuwapa tuzo na kuwafhamisha mila na tamaduni katika programu.

Successful Families 2020 ina shirikiana na wilaya ya shule ya **David Douglas School District** kuhimiza mazingira imara ya shule na kuhakikisha kuwa wanafunzi wasiokuwa weupe wanafuzu shule ya upili wakiwa tayari kwa chuo kikuu na kazi.

United Way ya Columbia-Willamette na Portland State University wanashirikiana na haya mashirika yasiyokuwa ya biashara na hizi shule pia ili kufahamu zaidi jinsi programu zao zinasaidia wanafunzi ndani na nje ya shule. Ili tuweze kufahamu zaidi kuhusu yale wanafunzi na wazazi/walezi walipitia katika programu hizi, tungependa kupata idhini yako ya kupokea maelezo ya elimu kuhusu watoto na vijana katika programu hizi.

Tunakusanya maelezo kupitia huduma ya elimu ya Multnomah County Education Service District kwa miaka ya shule 2016-2017, 2017-2018, na 2018-2019 ya wanafunzi wa shule za Earl Boyles Elementary School, Mill Park Elementary School, Ron Russell Middle School, David Douglas High School.

Kupatiana maelezo ya wanafunzi ya elimu na shule ni kwa hiari. Ukipendelea kutusaidia, tafadhali tia sahihi fomu ya idhini iliyoko kwenye pakiti hii.

**ASANTE KWA WAKATI WAKO!**

## Maelezo ya Idhini

**Nyaraka zifwatazo zinaeleza idhini zinazopeanwa na wazazi, walezi na wanafunzi. Kama unakubali, tia sahihi ukurasa wa mwisho wa Fomu ya Idhini.**

**Kama mwanafunzi na mzazi/mlezi pamoja wanatia sahihi fomu hii, una:**

- ☐ **Unaturuhusu kutazama na kutumia rekodi zako za mwanafunzi kama vile za kuhudhuria shule, matokeo ya mitihani, alama za mitihani, nidhamu na kufuzu**

- ☐ **Unaturuhusu kutumia rekodi za programu/huduma za Familia Zinazofaulu 2020 ambazo washiriki huenda wanazo kukuhusu (mwanafunzi na/au familia) ili kutuwezesha kuelewa vyema yale muliyoyapitia**

- ☐ **Fahamu kwamba hakuna majibu ya udadisi wa mtu yoyote binafsi (mwanafunzi au mzazi) yataonyeshwa wengine hadharani na hayataonyeshwa walimu, wafanyikazi wa shule, wazazi wengine na wafanyikazi wa mashirika yasiyokuwa ya biashara**

- ☐ **Tupatie (wahudumu na wadadisi) ruhusa ya kutumia picha au video zozote za wanafunzi na/au wazazi/walezi kwenye vifaa vya maelezo ya ufahamu.**

- ☐ **Fahamu kwamba kupatiana maelezo ya elimu ya wanafunzi ni kwa hiari, na unaweza kuwacha wakati wowote kwa kuwasiliana na Alejandro Queral kwa 503-226-9357**

# Fomu ya Idhini

Idhini Fahamu ya Jumla, ikiwa ni pamoja na kupatiwa rekodi za wanafunzi kwa utafiti huu:
***FanikiwaJamii 2020- Promise Neighborhood Initiatives***

Utafiti huu unahusu wanafunzi na familia ambao wao ni sehemu ya programu za usaidizi wa elimu na tamaduni (kama zile zinazopeanwa na Immigrant and Refugee Community Organization, Latino Network, Metropolitan Family Service, Native American Youth and Family Center na Self-Enhancement, Inc.) Wazazi/walezi na mwanafunzi wao wamekaribishwa kushiriki kwa sababu mwanafunzi amesajiliwa katika moja ya programu hizi.

Tunaomba ruhusa tutazame rekodi za masomo za mwanafunzi, ambazo huenda zitajumuisha kitambulisho cha mwanafunzi, darasa alilofikia, anavyohudhuria shule, matokeo ya mitihani, alama anazopata, hali ya kiuchumi, matokeo ya mitihani ya kupima uwezo wa masomo, nidhamu na kufuzu. Tunakusanya maelezo kwasababu tumeombwa na Idara ya Huduma za Binadamu ya Multnomah County (Multnomah County Department of Human Services) tuwapatie maelezo kuhusu maendeleo na mafanikio ya wanafunzi wanaoshiriki katika miradi shirika ya Successful Families 2020 katika shule zifwatazo: Earl Boyles Elementary, Mill Park Elementary, Ron Russell Middle School na David Douglas High School.

Tutatazama rekodi za wanafunzi kwa mwaka huu wa masomo (2016-2017), kwa miaka miwili ijayo ya masomo (2017-2018 na 2018-2019), na kwa mwaka wanaotazamiwa kufuzu shule ya upili. Huenda tutatumia vifaa vyengine kama utafiti ili kukusanya maelezo siku zijazo Rekodi nyengine za shule, na pia chochote ambacho mzazi au mwanafunzi anatwambia kwenye udadisi, kitawekwa kwa usiri. Ni wahudumu na wadadisi pekee ambao ni sehemu ya utafiti huu watakaoweza rekodi na majina ya yeyote yule. Hatutapatiana majibu yoyote yenye majina ya wahusika au maelezo binafsi ya mzazi au mwanafunzi na walimu, wafanyikazi wa shule, wazazi wengine, au wafanyikazi wa mashirika ya jumuiya yanayofanya kazi na mwanafunzi.

Tungependa kupatiana picha na video za wanafunzi/au wazazi wanaoshiriki kwenye programu shirika za Successful Families 2020 katika shule hizi. Kwa kutia sahini idhini hii, mwanafunzi na mzazi wanaruhusu na wanakubali kuwa IRCO, Latino Network, Metropolitan Family Service, Native American Youth and Family Center, Self-Enhancement, Inc. na United Way of the Columbia-Willamette wana haki miliki, kuchapisha, kutumia, kuuza au kutumia zozote au zote kati ya picha za uso (portraits) au filamu, kanda za video, na/au rekodi za sauti ambazo wamerekodi au wametengeza kuanzia tarehe hii, iwe ni kando na au pamoja na, mambo ya michoro au maandishi yaliyochapishwa, hadithi au habari, matumizi ya mtandao, kutokea katika televisheni/redio, au kwa matangazo, matangazo ya biashara au kwa madhumuni mengine yasiyovunja sheria. Sahihi yako (mzazi/mlezi) inaondosha madai yote ya malipo aina yoyote kwa matumizi aina hii na inaondosha haki yoyote ya kukagua na/au kuidhinisha kazi iliyokamilika ya maandishi ya matangazo ambayo huenda itatumika pamoja na picha au video ambapo mzazi au mwanafunzi wametokea. Kama haukubaliani na mapendekezo ya kupatiana picha na video kwa washirika hawa, unaweza kujiondoa kwa kuweka alama kiboksi cha kujiondoa katika sehemu ya kuweka sahihi ya fomu hii ya idhini.

Uamuzi wako wa kupatiana maelezo na picha za familia yako ni wa hiari. Unaweza kuamua kuacha kupatiana rekodi wakati wowote bila uamuzi huo kutatiza uhusiano wa mzazi au kijana na shirika la jamii, shule, au United Way ili waweze kushiriki katika programu zinazopeanwa na shirika lako la jamii.

Kama yeyote kati yenu ana maswali kuhusu ombi hili la maelezo, awasiliane na Alejandro Queral kwa 503-226-9357.

IDHINI YA MZAZI : Kwa kutia sahihi kwenye kisanduku cha manjano hapo chini, unasema kwamba unaelewa maelezo yaliyoaindikwa hapa juu, kwamba unapeana idhini mtoto/kijana wako apatiane rekodi zake za masomo na huduma kwa wafanyikazi na wadadisi wa programu wanaoshughulika na mradi wa Successful Families 2020- Promise Neighborhood Initiative. Unakubali pia kuidhinisha kutolewa na kubadilishwa kwa maelezo ya mwanafunzi wako ikiwa pamoja na jina, # ya kitambulisho, darasa lake, matokeo ya mitihani, alama za masomo, hali ya kiuchumi, kuhudhuria, na nidhamu katika ya Reynolds School District, Portland State University, United Way of Columbia-Willamette, na wafanyikazi wa utafiti na udadisi wanaofanya utafiti huu.

Jina la Mzazi/Mlezi (Andika) | Sahihi ya Mzazi/Mlezi | Tarehe

Jina la Mwanafunzi (Andika)

KUKUBALI KWA MWANAFUNZI: **Kwa kutia sahihi kwenye kisanduku cha manjano hapo chini, unasema kwamba unaelewa maelezo yaliyoaindikwa hapa juu.**

☐ *Tafadhali weka alama kama wewe, mwanafunzi, una zaidi ya miaka 18.*

Jina la Shule | Sahihi ya Mwanafunzi | Tarehe

KUJITOA KWENYE UPEANAJI PICHA/VIDEO:

☐ *Tafadhali chagua kiboksi hichi kama unapendelea kujitoa kwenye upeanaji picha/video.*

JINA LA MTAFSIRI/SHIRIKA: **Kwa kutia sahihi kwenye kisanduku cha manjano hapo chini, unathibitisha kuwa maelezo ya hapo juu yameelezewa Mzazi na Mwanafunzi kikamilifu kwa lugha wanayoelewa na kuwa maswali yao yamejibiwa.**

Jina la Mtafsiri, Shirika | Sahihi ya Mtafsiri | Tarehe